East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 2, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 2, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya

*Ann Wambui Gitau[1*] Eric W. Wamalwa[1] na Stanley Adika Kevogo[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Kibabii, S. L. P. 1699-50200, Bungoma, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, S. L. P. 210 - 40601 Bondo, Kenya.
[*] ORCID: https://orcid.org/0000-0003-4887-2521; Barua pepe ya mawasiliano: anngitau1963@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*19 Desemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ufundishaji wa Masuala Mtambuko, Mtaala wa umilisi, Ujifunzaji.*

## IKISIRI

Masuala mtambuko ni baadhi ya mambo muhimu yanayofundishwa katika mtaala wa elimu. Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya imejumuisha na kusisitiza ufundishaji wa masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi. Isitoshe, masuala mtambuko yanajitokeza kuwa muhimu sana katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika shule za msingi. Hata hivyo, tafiti zimebaini kuwa ufundishaji haujatekelezwa inavyostahili. Makala haya yanatathmini ufundishaji wa masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili wa shule za msingi za kaunti ndogo ya Kimilili. Nadharia ya Utekelezaji wa Uvumbuzi iliyoasisiwa na Gross na wenzie (1971) imetumika. Walimu 38 walishirikishwa katika utafiti. Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji na uchunzaji. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba, walimu walitumia mbinu mbalimbali za ufundishaji kwa viwango tofauti. Asilimia100 ya walimu walitumia mbinu ya maswali na majibu kufundisha masuala mtambuko. Aidha, asilimia 63 walitumia majadiliano; nayo asilimia 49 ya walimu walitumia mbinu ya vikundi vya ushirika  Baadhi ya mbinu zilitumika kwa uchache tu na nyingine hazikutumika kabisa. Licha ya hayo, mbinu zilizotumiwa katika ufundishaji hazikutumiwa kwa ufanisi mkubwa. Aidha matokeo yameonesha kwamba walimu walikumbwa na changamoto katika uteuzi na matumizi ya mbinu mwafaka za ufundishaji wa masuala mtambuko. Kutokana na matokeo haya, inapendekezwa kuwa, warsha za mara kwa mara ziandaliwe kwa walimu walio nyanjani kwa minajili ya kuwanoa na kuwapiga msasa kuhusu utekelezaji wa ufundishaji wa mtaala wa elimu ya umilisi, na matumizi ya vifaa mwafaka vya kufundishia vikiwemo vifaa halisi na vya kielektroniki. Pili, inapendekezwa kuwepo kwa tathmini ya mara kwa mara kuhusu ubora na kiwango cha ufundishaji wa masuala mtambuko na utekelezaji wa mtaala wa umilisi  katika shule za msingi.

**APA CITATION**

Gitau, A. W., Wamalwa, E. W. & Kevogo, S. A. (2023). Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(2), 73-83. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

**CHICAGO CITATION**

Gitau, Ann Wambui, Eric W. Wamalwa and Stanley Adika Kevogo. 2023. "Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 73-83. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645.

**HARVARD CITATION**

Gitau, A. W., Wamalwa, E. W. & Kevogo, S. A. (2023) "Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 73-83. doi: 10.37284/jammk.6.2.1645.

**IEEE CITATION**

A. W. Gitau, E. W. Wamalwa, & S. A. Kevogo "Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 73-83, Dec. 2023.

**MLA CITATION**

Gitau, Ann Wambui, Eric W. Wamalwa & Stanley Adika Kevogo. "Tathmini ya Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Dec. 2023, pp. 73-83, doi:10.37284/jammk.6.2.1645.

## UTANGULIZI

Elimu inayofundishwa darasani inaendelea kupanuka kimataifa kadiri masuala yanavyochipuka katika jamii kila kukicha. Jamii zinazidi kukumbwa na hali na matukio mbalimbali ambayo hulazimu kuangaziwa katika mipango ya kielimu (UNESCO, 2000). Kwa sababu hii, masuala mtambuko hayawezi kuepukika, kwani mwanafunzi hutangamana nayo kila siku ndani na nje ya shule. Kwa hivyo, elimu haina budi kuyashughulikia masuala mtambuko pamoja na changamoto zinazotokana nayo. Matokeo ya ufundishaji yanapaswa kuchochea mabadiliko miongoni mwa wanafunzi na wanajamii kwa jumla kuhusiana na masuala mtambuko. Kwa hali hiyo, maarifa, stadi na maadili yanayofundishwa darasani yanastahili kuwa na umuhimu kwa wanafunzi katika kushughulikia changamoto zinazotokana na masuala mtambuko (UNESCO, 2000).

Schleicher (2018) anaishadidia hali hii anapohoji kuwa mifumo ya elimu inapaswa kukabiliana na mabadiliko yanayoibuka katika jamii ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu itakayowategemeza katika kuboresha ujuzi, ufahamu, mitazamo na maadili yatakayowafaa katika maisha baada ya shule.

Mtaala wa Umilisi umedhamiriwa kutoa elimu itakayomfaa mwanafunzi katika ukuzaji wa uwezo wa kutumia ujuzi na maarifa ayapatayo shuleni katika kutekeleza shughuli mbalimbali katika jamii (Sifuna & Obonyo, 2019). Kwa mujibu wa shirika la UNICEF (1999) elimu ni kani muhimu katika kufanikisha mabadiliko ya kijamii. Aidha, elimu ni nyenzo muhimu katika kupambana na umasikini, kulinda haki za watoto, kuendeleza haki za kibinadamu na demokrasia, kutunza mazingira pamoja na kuthibiti ongezeko la idadi ya watu. Ni katika misingi hii ambapo dhima ya elimu katika kujishughulisha na masula mtambuko katika jamii inadhihirika.

Kupitia kwa elimu, wanajamii hukombolewa kutokana na hali yao ya asili kama vile ujinga, umaskini, magonjwa, ubinafsi, hofu, ufisadi, udhalimu, utumwa, kupotoka kimaadili na hali nyinginezo tenge (Chang'ach & Kessio, 2012). Ufikiwaji wa malengo ya ufundishaji yanayohusiana na masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika elimu ya shule za msingi nchini Kenya unahitaji ushirikiano wa mwalimu na mwanafunzi katika mchakato wa ufundishaji (KICD, 2017). Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya (2017) imefanya juhudi kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa mtaala wa umilisi umefanikiwa. Licha ya juhudi hizo, uchunguzi kuhusu utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi unaonyesha kuwa ufundishaji wa masuala mtambuko haujatekelezwa ipasavyo (Ondimu, 2018; Sifuna & Obonyo, 2019; Owala, 2021). Isitoshe, masuala mtambuko yanajitokeza kuwa muhimu sana katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya. Makala haya yanadhukuru ufundishaji wa masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika shule za msingi. Baaddhi ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

maswali yaliyotafutiwa majibu katika uchunguzi huu yalikuwa; Je, maswala mtambuko hufundishwa katika mtaala wa umilisi? Iwapo yananafundishwa, walimu hutumia mbinu zipi kuyafundisha? Je, mbinu hizo hufaulisha ufundishaji wa masuala mtambuko?

## HAKIKI WA MAANDISHI

Karne ya 21 inakumbwa na changamoto za kijamii, kisiasa, na kiuchumi kama vile: uendelevu wa mali asili, ustawishaji wa uchumi wa taifa, uboreshaji wa afya ya jamii, na maadili mema pamoja na uhifadhi wa mazingira (NCPPHE, 2008). Kutokana na hali hii sekta ya elimu haina budi kushughulikia masuala ya kijamii. Wazo hili linaendana na dhima ya elimu katika kushughulikia masuala mtambuko ili kupata suluhu la kudumu kuhusiana na changamoto za kijamii. Isitoshe, mojawapo ya mahitaji ya msingi ya mwanafunzi wa karne ya 21 ni umilisi unaomwezesha kutafakari na kufikiri kwa kina. Maarifa ambayo wanafunzi wanayapata shuleni yanastahili kuwawezesha kutatua matatizo ya kesho kwa kufanya maamuzi kimantiki na kushiriki katika utatuzi wa matatizo ya kimaisha ya muda mrefu (Ndege na wenzie, 2020). Kadri masuala mtambuko yanavyoendelea kutanuka na kupanuka, ndivyo umuhimu wa waelimishaji kufahamu namna ya kushughulikia mahitaji ya wanafunzi kikamilifu unapata umaarufu (Ransaw & Majors, 2017). Makala hii inatathmini mbinu zinazotumiwa na walimu katika kushughulikia masuala mtambuko.

Baadhi ya masuala mtambuko muhimu yanayopaswa kufundishwa katika Mtaala wa Umilisi wa somo la Kiswahili ni uraia. Suala hili linaelimisha wanafunzi kuhusu amani, uaminifu, utawala bora, ushirikiano wa kijamii, uzalendo, haki za watoto, huduma, na ulinzi kwa watoto. Pia, kuna elimu ya afya. Suala hili linahusu VVU na ukimwi, kudhibiti ulevi na matumizi ya dawa za kulevya, magonjwa yanayotokana na mtindo wa maisha, usafi, magonjwa ya kawaida ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, na magonjwa sugu. Aidha, kuna stadi za maisha na elimu ya maadili ambalo hujumuisha elimu ya stadi za maisha, maadili ya msingi na jinsia ya binadamu. Isitoshe, kuna suala la elimu kwa maendeleo endelevu (EME) ambalo linahusu elimu ya mazingira, kupunguza hatari za maafa, elimu ya usalama, elimu ya fedha, kumaliza umaskini, kupambana na ugaidi, machafuko na ukandamizaji, masuala ya jinsia, na elimu ya ustawi wa wanyama. Aidha mwanafunzi anahimizwa kushiriki katika shuguli za huduma za kijamii ambazo kwazo atajifunza mambo mengi (KICD, 2017; Ndege na wenzie., 2020).

Ufundishaji bora wa masula mtambuko unalenga kuboresha stadi, ufahamu na maadili ambayo yatamwezesha mwanafunzi katika kushughulikia masuala muhimu katika maisha yao na jamii. Mbinu zitakazotumiwa kufanikisha ujifunzaji zinaweza kuimarisha msisitizo wa masuala haya au zikakwamisha juhudi zilizowekwa kuhakikisha masuala mtambuko hayapuuzwi (KICD, 2017). KICD inatilia mkazo matumizi ya mbinu bora za ufundishaji wa masuala mtambuko ili kukuza umilisi mwafaka miongoni mwa wanafunzi ambao utaiwezesha jamii kunawiri katika kila nyanja. Hata hivyo, upungufu au hata ukosefu wa nyenzo za kuelekeza ufundishaji, mathalan vitabu bora vya kiada, umezua changamoto katika utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi (Owala, 2021). Hali hii inamaanisha kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa masuala mtambuko katika mtaala wa Kiswahili kwenye shule za msingi kama mojawapo ya yaliyomo katika Mtaala wa Umilisi wa shule za msingi vile vile umeathirika kwa njia hasi; kwani, mbinu na nyenzo za ufundishaji huwezeshwa na uteuzi pamoja na matumizi bora ya nyenzo za ufundishaji.

Isitoshe, ukosefu wa maarifa na stadi mwafaka katika matumizi ya teknolojia katika ufundishaji miongoni mwa walimu ni mojawapo ya changamoto zinazokabili utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi (Ondimu, 2018). Akitaja umuhimu wa matumizi ya teknolojia, Owala (2021) anaohoji kuwa, wakati teknolojia inatumiwa kama nyenzo ya ufundishaji, huwezesha walimu na wanafunzi kupata maarifa mapya, stadi, mitazamo na maadili ambayo huimarisha matokeo ya ufundishaji. Mbinu na vifaa vya ufundishaji huathiriana ili kufanikisha ufundishaji. Vifaa mwafaka

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

huimarisha mbinu za ufundishaji, hivyo kuwezesha ufikiaji wa malengo ya ufundishaji. Maelezo ya Ondimu (2018) na Owala (2021) yanadhihirisha kuwepo kwa changamoto katika matumizi ya mbinu mwafaka za ufundishaji, hivyo basi mbinu za ufundishaji vile vile ziliathirika. Upungufu wa maarifa na ujuzi ulikuwepo kuhusiana na Mtaala wa Umilisi miongoni mwa walimu na walimu wakuu kwa sababu hawakupata mafunzo ya kutosha kuhusiana na utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi; dhihirisho kwamba walimu walikuwa na maarifa na ujuzi haba wa kufanikisha utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi (Sifuna & Obonyo, 2019). Makala haya yametathmini ufaafu wa mbinu za ufundishaji wa masuala mtambuko katika mtaala wa umilisi wa shule za msingi.

## MISINGI YA NADHARIA

Nadharia ya utekelezaji uvumbuzi wa mtaala ilitumika. Nadharia hii iliasisiwa na Gross na wenzake (1971). Nadharia hii inahoji kwamba utekelezaji wa mtaala wowote unategemea uwepo wa mahitaji mwafaka ya utekelezaji. Ili kujenga nadharia hii, waasisi hawa walichunguza utekelezaji wa majaribio ya uvumbuzi wa mtaala katika shule ya msingi Cambire. Lengo lao lilikuwa kubaini mambo ambayo yanaweza kuzuia utekelezaji wa uvumbuzi wa mtaala. Wataalamu hawa waligundua kuwa kutofaulu kwa utekelezaji wa uvumbuzi ulioanzishwa kunatokana na matatizo ambayo yalijitokeza wakati wa majaribio ya utekelezaji na ambayo hayakutatuliwa. Gross na wenzie, (1971) wamenukuliwa na Nyokabi (2018) anayeorodhesha mihimili mitano inayofanikisha zoezi la utekelezaji wa uvumbuzi wa mtaala.

Mhimili wa kwanza ni Ufahamu wa Yaliyomo. Utekelezaji wa ufundishaji unategemea kiwango ambacho watekelezaji watapata ufahamu na uelewa wa mtaala. Mhimili wa pili ni Uwezo wa Mtekelezaji. Uwezo wa mtekelezaji ni ufahamu na maarifa yanayohitajika katika kutekeleza mtaala. Mhimili wa tatu ni Vifaa na Nyenzo. Vifaa na mbinu hutegemeana katika utekelezaji wa ufundishaji hivi kwamba, mbinu teule itafaa tu iwapo vifaa mwafaka vitatumika. Mhimili wa nne ni Mipangilio ifaayo. Mipangilio kuntu inayoambatana na mtaala unaopaswa kutekelezwa. Mipangilio hii inahusiana na uratibu wa masomo. Mhimili wa mwisho ni Kujitolea. Kufaulu kwa utekelezaji wa mtaala unategemea kiwango ambacho wahusika watekelezaji watajitolea. Kutofaulu kwa utekelezaji wa mtaala aghalabu hutokana na mikakati inayotumiwa na wale wanaoongoza mchakato wa utekelezaji wa mitaala. Mikakati hii huwa haipimi na kukisia changamoto ambazo huenda zikatokea katika utekelezaji wa mitaala mipya.

Utafiti huu ulitumia mihimili mitatu kati ya hii mitano. Mhimili wa kwanza, ufahamu wa yaliyomo, ulitumika katika kufikia lengo linalohusu utambuzi wa masuala mtambuko yanayofundishwa katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika shule za msingi zipatikanazo katika kaunti ndogo ya Kimilili. Mhimili huu uliwezesha kubaini ufahamu wa walimu kuhusu masuala yanayopaswa kufundishwa pamoja na maudhui yapaswayo kushughulikiwa chini ya mada zilizoteuliwa kuhusu masuala mtambuko.Vilevile, mhimili wa kwanza ulitumika kufikia lengo la tatu. Mhimili huu ulitumiwa kutathmini iwapo walimu walitumia ubunifu unaofaa katika kuteua mbinu faafu za kufundisha masuala mtambuko yanayopaswa kufundishwa katika Mtaala wa Umilisi katika somo la Kiswahili. Ilichunguzwa iwapo walitumia ubunifu katika kufikia malengo ya ufundishaji wa yale masuala mtambuko. Mhimili wa pili ulitumika kufikia lengo la pili. Mhimili huo ulituwezesha kufafanua ufaafu wa maarifa ya walimu katika uteuzi wa mbinu za ufundishaji wa masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili. Mhimili wa tatu ulitumika kubainisha vifaa vilivyotumiwa na walimu katika ufundishaji na jinsi vilivyotumika katika kuwezesha mbinu za ufundishaji wa masuala mtambuko.

## MBINU ZA UTAFITI

Uchunguzi huu ulitumia muundo wa uchunguzi wa kifani mkabala wa kithamano. Kwa mujibu wa Kumar (2005) muundo wa utafiti ni kielelezo na mikakati ya uchunguzi ambayo mtafiti anatumia katika kupata majibu ya maswali ya utafiti. Utafiti

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

huu ulifanywa katika shule za msingi katika kaunti ndogo ya Kimilili, kaunti ya Bungoma. Shule 26 ziliteuliwa kinasibu na kushirikishwa katika utafiti kati ya shule 85 za msingi katika kaunti ndogo ya Kimilili.

Walengwa wa utafiti walikuwa walimu wote (170) wa somo la Kiswahili wa darasa la nne na la tano katika Kaunti ndogo ya Kimilili. Hata hivyo, sampuli ya walimu 38 wa gredi ya nne na tano waliteuliwa kimakusudi ili walishirikishwe katika ukusanyaji wa data

Njia zilizotumiwa katika kukusanya data ni hojaji na uchunzaji. Kwa hivyo, vifaa vilivyotumiwa kufanikisha ukusanyaji wa data yenyewe vilikuwa Mwongozo wa Uchunzaji na Hojaji Huru. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu mseto. Matokeo yamewasilishwa kwa kutumia maelezo, takwimu, na jedwali.

## MATOKEO NA MJADALA

Ili kufanikisha tathmini ya mbinu zilizotumiwa kufundisha masuala mtambuko, mbinu zilizotumiwa na walimu wa somo la Kiswahili darasani kufikia malengo ya ufundishaji zilichunzwa. Utafiti ulilenga kubaini matumizi ya mbinu hizi katika ufundishaji wa masuala mtambuko. Iligunduliwa kwamba walimu hawakuonyesha ufahamu wa mbinu bora zinazostahili katika ufundishaji wa masuala mtambuko katika Mtaala wa Umilisi wa Kiswahili katika shule za msingi. Walimu wengi walitumia mbinu za kimapokeo katika ufundishaji wa masuala mtambuko.

**Jedwali 1: Mbinu zilizotumiwa Kufundishia Masuala Mtambuko**

| **Mbinu** | **Masuala Mtambuko na Idadi ya walimu** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Ukimwi** | **Mazingira** | **Haki za Watoto** | **Umaskini** |
| Vikundi vya Ushirika | 12 (40%) | 20 (67%) | 12 (40%) | 15 (50%) |
| Majadiliano | 20 (67%) | 22 (73%) | 18 (60%) | 15 (50%) |
| Uigizaji | 00 (0%) | 00 (0%) | 00 (0%) | 00 (0%) |
| Maswali na Majibu | 30 (100%) | 30 (100%) | 30 (100%) | 30 (100%) |
| Ziara Nyanjani | 00 (0%) | 04 (13%) | 00 (0%) | 02 (7%) |
| Nyimbo | 02 (7%) | 05 (17%) | 04 (13%) | 04 (13%) |
| Mhadhara | 30 (100%) | 30 (100%) | 30 (100%) | 30 (100%) |
| Kazi mradi | 00 (0%) | 00 (0%) | 00 (0%) | 00 (0%) |

**Chanzo**: Data ya Nyanjani (2022)

Data iliyochanganuliwa inaonyesha kuwa, walimu wote 30 waliosailiwa, ikiwa ni 100% walitumia mbinu zifuatazo katika ufundishaji wa masuala mtambuko: ‘Mbinu ya Maswali na Majibu’ na ‘Mbinu ya Mhadhara’ katika gredi ya Nne na ya Tano. Data iliyopatikana kupitia hojaji huru kwa walimu ilithibitishwa kwa uchunzaji darasani. Ilidhihirika kuwa mbinu zilizotumiwa sana katika ufundishaji wa masuala yote manne yaliyochunguzwa katika gredi zote mbili zilikuwa: ‘Maswali na Majibu’ na ‘Mhadhara’. mbinu hizi mbili zilitumiwa na walimu wote 30 (100%) walioshiriki.

Mbinu za ufundishaji zinastahili kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli za ufundishaji. Pia, mbinu mwafaka zinastahili kuwapa wanafunzi fursa ya kutoa mchango wao wakati wa ufundishaji. Aidha, mwalimu anatakiwa kuwa na mlahaka mwema na mwanafunzi ili kumjengea mwanafunzi mazingira mema yatakayoimarisha ujifunzaji na kutumia mbinu mwafaka za ufundishaji zitakazoathiri mwanafunzi kimawazo kwa kumwezesha kujifunza hivyo kuwezesha ufikiaji wa malengo ya ufundishaji (Kassem, 1992). Anaeleza kwamba malengo ya somo yanastahili kulenga mahitaji mbalimbali ya wanafunzi ilhali mbinu za ufundishaji zifahamike vyema ili kuimarisha ujifunzaji. Kinyume na maelezo ya Kassem, mbinu ya mhadhara na maswali na majibu hazikuwezesha ufikiaji wa malengo ya ufundishaji wa masuala mtambuko ambayo ni ukuzaji wa umilisi mwafaka miongoni mwa wanafunzi.Walimu wote 30, (100%) walioshiriki katika utafiti huu walibainika kutumia mbinu za ‘Maswali na Majibu’ pamoja na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

mbinu ya 'Mhadhara' katika ufundishaji wa masuala mtambuko yote.

**Mbinu ya Maswali na Majibu**

Mbinu ya maswali na majibu humhitaji mwalimu kutumia maswali ili kuwafanya wanafunzi wafikiri kwa kina na kutafakari yanayofundishwa. Mwalimu pia huhitajika kuwapa muda wa kufikiri, kujadiliana na kuandika baadhi ya hoja zinazoibuliwa wakati wa kutoa majibu (Ndege na wenzie, 2020).

Kuptia mbinu hii, mwalimu anatarajiwa kuandaa maswali kabla ya somo na baadaye awape wanafunzi muda wa kufikiri kwa kina pamoja na kuhusisha mbinu zinginezo kama vile vikundi vya ushirika na majadiliano ili wapate hoja watakazoziibua darasani. Ina maana kuwa, mbinu za ufundishaji hushirikiana na kuathiriana katika kufaulisha mchakato wa ufundishaji na hatimaye kufikia malengo ya ufundishaji. Japo walimu walitumia mbinu hii, ilidhibitishwa kuwa, wanafunzi hawakupata muda wa ziada wa kujiandaa kabla ya somo. Walimu walikiri kuwa hawakuwa na muda wa kutosha kuwaanda wanafunzi kutafitia suala husika kama ilivyorajiwa ili kufanikisha ufundishaji kwa kuhusika katika kujibu maswali darasani.

Mbinu ya maswali na majibu pia inaweza ikatumika katika kipindi kimoja tu; ambapo mwalimu anatarajiwa kuandaa swali dadisi moja tu ambalo linahitajika kuendesha kipindi chote kupitia michango ya wanafunzi. Hivi, swali dadisi hutarajiwa kumwelekeza mwanafunzi katika kujibu maswali anayoyajua na hatimaye kupata ujuzi, maarifa, ufahamu na umilisi mpya (Ndege na wenize, 2020). Mbinu hii huwaelekeza wanafunzi katika kuchangiana maarifa wenyewe kwa wenyewe. Mbinu hii vile vile inatarajiwa kumjengea mwanafunzi uwezo wa kufikiri kwa kina na kutatua matatizo kwa vile inachochea kuwaza kwa kina miongoni mwao na kutafakari kuhusu mada teule. Hivyo basi, ni jukumu la mwalimu kuwa na subira ili kuyadhibiti mawazo wanafunzi kupitia udadisi hadi afikie kilele ambapo ataibua jibu sahihi.

Ingawa walimu wengi walitumia mbinu ya maswali na majibu, uchunzaji ulionyesha kuwa walipungukiwa na ufahamu wa jinsi ya kuitumia ili kuboresha ufundishaji. Mbinu hii iliwashirikisha wanafunzi wachache, hususan wale walioonekana kuelewa haraka na kujifunza yaliyomo kwenye somo kwa wepesi. Ingawa walimu walionekana wakiwauliza wanafunzi maswali, wanafunzi wenyewe hawakupata fursa wala muda wa kutosha kujadiliana na kuibuka na majibu yao wenyewe.

Mbinu ya maswali na majibu hunuiwa kumwezesha mwalimu kutathmini uzoefu alionao mwanafunzi kuhusiana na suala linalohusika; baada yao kutafiti, kujadili na kuibuka na jibu sahihi kuhusu suala husika. Hata hivyo, mwalimu hangefaulu katika kutathmini kikamilifu kwa kuwa wanafunzi wachache tu ndio walioshiriki katika kujibu maswali.

Maswali na majibu huwa mbinu mwafaka katika kupata mrejesho kuhusu umilisi uliokuzwa miongoni mwa wanafunzi kuhusu ziara za mafunzo; haswa katika ufundishaji wa suala la mazingira ambapo mwanafunzi huhitajika kutangamana na hali halisi katika mazingira yao. Matumizi haya hayakushuhudiwa wakati wa uchunzaji. Japo mbinu hii ilipendekezwa kutumiwa katika ufundishaji wa masuala mbalimbali, mwalimu anatarajiwa kuitumia kwa namna ambayo itawasisimua wanafunzi kuhusika katika kukuza umilisi mwafaka miongoni mwao na kufikia malengo ya ufundishaji. Mbinu ya maswali na majibu huwajengea wanafunzi umilisi ufuatao; mawasiliano na ushirikiano wanaposhirikiana katika majadiliano ili kupata jawabu la swali husika kuhusu suala teule. Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo pia hukuzwa miongoni mwa wanafunzi, wanapotafakari na kufikiri kwa kina kuhusiana na suala teule. Ujuzi wa kidijitali pia unakuzwa wanafunzi wanapotumia vifaa mbalimbali vya kidijitali kutafitia swali husika (Ndege & wenize, 2020). Mbinu hii pia humchochea mwanafunzi kujifunza zaidi. Ingawaje walimu waliitumia mbinu hii, haikufanikisha ufikiaji wa malengo ya ufundishaji kikamilifu. Uchunzaji ulionyesha

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

kuwa walimu waliwashirikisha wanafunzi wachache katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Mbinu ya Mhadhara**

Pamoja na mbinu nyinginezo, mbinu ya Mhadhara ilitumiwa na walimu 30 ikiwa ni 100% ya walimu katika kufundishia masuala mtambuko yote. Mbinu ya mhadhara si faafu kwa kufundishia wanafunzi wachanga kwa kuwa ni changamani, hivyo vigumu kuielewa. Japo mbinu hii ilitumika kwa wingi, haikuwafaa wanafunzi kwa kiasi kikubwa katika kiwango cha gredi ya nne na tano, ikizingatiwa kuwa ni wachanga. Matokeo haya yanaunga mkono kauli ya Mbae (2015) katika uchunguzi wake anapoeleza kwamba, walimu walikiri kuwa walitumia mbinu ya mhadhara katika kufundishia somo la Kiswahili katika shule za msingi. Anaongeza kuwa, mbinu hii haikuwafaa wanafunzi katika kiwango hiki. Hivyo basi wanafunzi hawakunufaika kutokana na mbinu hiyo na umilisi tarajiwa haungekuzwa miongoni mwao.

Pamoja na hayo, kwa maoni yetu, mbinu bora za ufundishaji katika shule za msingi, hususan ufundishaji wa masuala mtambuko ni zile zinazopaswa kumchangamsha mwanafunzi, hivyo kumchochea katika kushiriki katika somo. Mbinu hii haikuwashirikisha wanafunzi ilivyotarajiwa kwa vile mwalimu ndiye aliyezungumza kwa kiasi kikubwa.

Aidha, mbinu ya mhadhara huwachosha wanafunzi haraka kwa vile uhusika wao katika ufundishaji huwa finyu. Pamoja na hayo, mbinu ya mhadhara humzuia mwalimu kutathmini ifaavyo kwa kuwa haimshirikishi mwanafunzi inavyohitajika, hivyo ni vigumu kupima umilisi wao kuhusu suala husika. Katika uchunzaji wetu, mwalimu alionekana kutoa mchango wake zaidi kuhusiana na somo, hivyo wanafunzi hawakupata nafasi mwafaka ya kuwasilisha mawazo yao kuhusu suala husika.

Kwa mujibu wa KICD (2019), mbinu mwafaka za ufundishaji ni zile zinazomhusisha mwanafunzi kikamilifu, mwalimu akiwa mwezeshaji na mwelekezi katika ufikiaji wa maazimio ya ufundishaji; pamoja na kumfunza mwanafunzi jinsi ya kutatua matatizo yanayoibuka katika jamii. Kwa mujibu wa maelezo haya mbinu ya mhadhara inaibuka kutofaa katika ufundishaji wa masuala mtambuko katika viwango hivi.

**Mbinu ya Vikundi vya Ushirika**

Mbinu ya vikundi vya ushirika ilitumiwa na 40% ya walimu katika ufundishaji wa suala la UKIMWI na 67% kufundishia suala la Mazingira. 40% na 50% ya walimu walitumia mbinu ya vikundi vya ushirika katika ufundishaji wa suala la Haki za watoto na suala la Kukabiliana na umaskini, mtawalia. Mbinu ya vikundi vya ushirika ilitumika na 56% ya walimu kwa mujibu wa hojaji. Ina maana kuwa 44% hawakushirikisha mbinu hii katika ufundishaji wa masuala mtambuko. Mbinu hii haikutumika kamwe katika ufundishaji wa suala la kukabiliana na umaskini na haki za watoto. Kupitia mbinu hii, mwalimu anastahili kumshirikisha mwanafunzi katika kupata majibu ya maswali yanayotokana na masuala fulani husika. Hivyo basi ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kwamba mwanafunzi anashiriki ifaavyo ili kukuza umilisi tarajiwa. Hata hivyo, uchunzaji ulibainisha walitumia mbinu hii kwa uchache mno. walimu walikuwa wakiteua wanafunzi wachache tu walioonekana kuwa na ufahamu kuhusiana masuala mtambuko waliyoshiriki kutatua. Vikundi vya ushirika humpa mwanafunzi fursa ya kufahamu uwezo wao wa kutatua masuala yanayohusiana na somo linalofundishwa.

Mbae (2015) anashadidia hoja hii anapoeleza kuwa, mbinu ya vikundi vya ushirika ni mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kuwa huwashirikisha wanafunzi katika mijadala, mawasiliano, na mawasilisho kuhusiana na suala husika. Mbinu hii haikufaulisha ufundishaji wa masuala mtambuko kwa kuwa haikuwashirikisha wanafunzi wote katika ufundishaji na ujifunzaji. Ilitumiwa na walimu wachache tu katika ufundishaji wa masuala ibuka mawili kwa mujibu wa hojaji; suala la Ukimwi na 40% mazingira na 67% ya walimu, huku uchunzaji ukibaini matumizi yake na 34% na 22% katika ufundishaji wa suala la mazingira na Ukimwi mtawalia.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Ilibainika kuwa, 30% ya wanafunzi ndio walioshiriki katika kujibu maswali yaliyoibuliwa kutokana na masuala mtambuko. Hivyo 70% ya wanafunzi haikushiriki katika mchako wa ufundishaji na ujifunzaji kinyume na ilivyotarajiwa kupitia mbinu hii.

Mbinu hii inampa mwanafunzi fursa ya kufahamu uwezo wao wa kutatua masuala yanayohusiana na somo linalofundishwa. Mbinu hii inatarajiwa kujenga umilisi wa mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayohusiana na masuala mtambuko mbalimbali. Pia mbinu hii inaimarisha kiwango cha wanafunzi kujiamini wanapowasilisha matokeo yao. Mtaala wa Umilisi wa Kiwsahili umependekeza matumizi ya mbinu hii katika ufudishaji wa Kiswahili kwa jumla pamoja na kuangazia masuala mtambuko mbalimbali yanayoathiri jamii (KICD, 2019; Ndege na Wenzie, 2020).

**Mbinu ya Majadiliano**

Mbinu ya majadiliano aghalabu huwahusisha wanafunzi katika mchakato wa kubadilishana mawazo huku wakisimamiwa na mwalimu. Mbinu hii inamwezesha mwanafunzi katika kukuza mawazo mapya kupitia kwa michango ya Wenzie. Pamoja na hayo, mwanafunzi huweza kugandisha dhana muhimu, huchochea uvumbuzi mpya miongoni mwa wanafunzi, huimarisha ujasiri wa mwanafunzi kwa vile huhitajika kuwa na ushawishi kuhusiana na hoja fulani (Nyokabi, 2018). Ili kutumia mbinu hii mwalimu anastahili kutambua tatizo na kutathnimi iwapo linahitaji ushirikiano wa wanafunzi kimawazo ili kutafutiwa suluhu. Aghalabu, mchakato wa mawasiliano hunuiwa ujenzi wa umilisi na ujuzi mpya miongoni mwa wanafunzi kutokana na michango ya wenzao.

Kwa kawaida, ili kufanikisha mbinu ya majadiliano, mwalimu ana majukumu yake, hali kadhalika mwanafunzi. Mwalimu anastahili kuwaandaa wanafunzi mapema na kutayarisha kipindi cha kuwasilisha hoja zao. Aidha, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanadumisha nidhamu, kuwaelekeza kuhusiana na masuala mtambuko, kukadilia muda unavyotumiwa pamoja na kuwatathmini (Magare, 2011).

Walimu 67%, 73%, 60% na 50% walikiri kuwa walitumia mbinu ya majadiliano katika ufundishaji wa suala la Ukimwi, mazingira, haki za watoto na kukabiliana na umaskini mtawalia. 63% kwa wastani ndio waliotumia mbinu ya majadiliano katika ufundishaji wa masuala mtambuko. Ina maana kuwa, 37% ya walimu hawakutumia mbinu ya majadiliano katika kuwezesha ufikiaji wa malengo ya ufundishaji. Japokuwa 63% walimu walitumia mbinu ya majadiliano walidai kuwa, mbinu hii ilichukua muda mwingi hivyo hawakuweza kufikia malengo tarajiwa. Huenda huu ni upungufu kwa upande wa walimu unaoelekeza kuhusu ukosefu wa maandalizi bora.

Ili kutathmini uelewa wa wanafunzi pamoja na kufaulu kwa mbinu hii; mwalimu anastahili kuhakikisha kuwa, kila mwanafunzi anashiriki katika mawasilisho. Hata hivyo, wanafunzi wachache ndio walioonekana wakishiriki.

Mbinu ya majadiliano ikitumika ipasavyo inakuza umilisi miongoni mwa wanafunzi ambao huimarisha viwango vyao vya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na masuala mtambuko katika jamii. Umilisi huu ni kama vile: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu na uraia. Matumizi ya mbinu hii haikufanikisha ujuzi wa umilisi mwafaka miongoni mwa wanafunzi kuhusiana na masuala mtambuko kama ilivyotarajiwa..

**Mbinu Nyinginezo**

Mbinu zilizotumika kwa uchache zaidi ni ziara nyanjani na matumizi ya nyimbo. Kwa mujibu wa Wasike (2015), matumizi ya nyimbo katika ufundishaji wa masuala mtambuko huimarisha kumbukumbu za wanafunzi kuhusu mada inayohusika. Mbinu ya nyimbo huwasisimua wanafunzi kuhusu mada teule na kwa njia hiyo kuimarisha kumbukizi ya somo linalohusika. Hata hivyo, matumizi ya nyimbo yanamhitaji mwalimu kuwa makini kwa vile nyimbo pia zaweza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

kusisimua kumbukumbu ambazo huenda zikaibua hisia hasi mingoni mwa wanafunzi na hivyo kutoa mchango hasi kwa mwanafunzi. Mbinu hii ilitumiwa na 7% kufundishia suala la Ukimwi, 17% suala la mazingira na 13% kufundishia suala la haki za watoto na umaskini. 7% waliotumia mbinu hii kufundishia suala la Ukimwi waliitumia katika ufundishaji wa maudhui ya athari ya Ukimwi, Hata hivyo, Mbinu hii haikutumika kwa ufanisi katika kufundishia masuala mtambuko. Matumizi ya nyimbo katika ufundishaji wa masuala mtambuko yanahitaji ubunifu ili kuzuia kuibua hisia miongoni mwa wanafunzi kando na kukuza umilisi mwafaka.

Mbinu ya maigizo inahusisha wanafunzi ambao huhitajika kuchukua dhima ya mhusika fulani, kuiga na kutekeleza majukumu yake. Wanafunzi baadaye huongozwa na mwalimu katika kujadili maudhui katika igizo linalohusika. Igizo lenyewe hutathminiwa kabla ya mchezo wenyewe ili kuhakikisha kuwa linaimarisha uelewa wa mwanafunzi kuhusiana na suala linalohusika, pamoja na kukuza umilisi unaohusika miongoni mwao. Mwalimu pia anaweza kuboresha na kuimarisha umilisi wa wanafunzi kwa kuwahimizi wabuni kisa ambacho watakiigiza. Hivi, ubunifu na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi huimarika. Kupitia uigizaji mwanafunzi hutangamana na uhalisia wa mambo, na hivyo kugandisha dhana na kuimarisha ufahamu wake (Ndege na wenzie, 2020). Mbinu ya uigizaji aidha inaimarisha umilisi wa uwezo wa kutatua mambo katika hali halisi ambayo huenda wanafunzi wakakumbana nayo wakati wa kuigiza. Mbinu hii pia huimarisha ujasiri miongoni mwa wanafunzi. Mbinu hii ni bora katika ufundishaji wa masuala mtambuko kwa vile humpa mwanafunzi nafasi ya kukabiliana na matatizo na kwa njia hiyo kumweka katika uhalisia wa mambo yanayomkabili katika jamii. Hata hivyo walimu hawakuitumia kamwe.

Mbinu ya kazi mradi pia ni mojawapo wa mbinu bora za ufundishaji inapotumiwa vyema. Mbinu hii humhitaji mwalimu kugawanya mada inayohusika katika vijimada ambavyo wanafunzi hupaswa kuvishughulikia katika vikundi. Mbinu hii huimarisha ujifunzaji kwa kuchunguza, kutangamana na kuchangiana mawazo ambayo hukuza maarifa miongoni mwa wanafunzi kupitia kwa umahiri tofauti tofauti wa wanafunzi. Kisha wanafunzi huelekezwa na mwalimu katika kuwasilisha maoni yao. Mwalimu hufanya marekebisho ya hoja wanazowasilisha ili kuziboresha na kumjengea mwanafunzi umililisi kuhusu suala linalohusika.

Kando na tathmini ya muda mrefu; kama wanavyoamini walimu, mbinu hii huweza pia kutumika katika kipindi kimoja; ila mwalimu anapojiandaa vyema kwa ajili ya kipindi. Mbinu hii huvumbua uwezo wa awali wa mwanafunzi ambao hutumika kama wenzo katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa maarifa mapya, kupitia kipindi husika. Ili kufanikisha matumizi ya mbinu hii, wanafunzi wanapaswa kuteuwa mambo ya kushughulikia kuhusu suala fulani kwa kuelekezwa na mwalimu. Mwalimu anastahili kuwaelekeza wanafunzi katika kufahamu mambo wanayostahili kufanya ili kufanikisha mbinu hii. Njia hii inawezesha ukuzaji wa umilisi mbalimbali miongoni mwa wanafunzi kama vile: uwazaji kina, kujiamini na utatuzi wa matatizo. Japo mbinu ni faafu katika ufundishaji wa masuala mtambuko, walimu hawakuitumia katika ufundndishaji.

Mbinu ya ziara za mafunzo ilitumika kufundishia masuala mtambuko japo na walimu wachache tu, asilimia 13% na 7% katika ufundishaji wa suala la mazingira na kukabiliana na umaskini mtawalia. Mwalimu alihitajika kuandaa ziara ya kielimu inayojikita katika somo linalohusika. Kabla ya ziara, mwalimu alihitajika kuzuru eneo ili kuhakikisha kuwa mazingira hayo yangewafaa wanafunzi katika kuimarisha ufahamu, ujuzi na kukuza umilisi mwafaka miongoni mwa wanafunzi; pamoja na kuhakikisha usalama wao. Hata hivyo, kupitia mahojiano nao, ilidhihirika kuwa walimu hawakufanya maandalizi yoyote, hivyo kuzuia ufikiaji wa malengo ya ufundishaji kikamilifu. Ziara hizi zinaweza kuwa nje au ndani ya shule, kutegemea suala teule. Mbinu hii inamhitaji mwalimu kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua mambo muhimu na kuyanakili

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

au kuyarekodi ili kupata mrejesho kuhusiana na uvumbuzi ziarani. Mwalimu hutumia maswali na majibu ambayo yaamfaa katika kupima umilisi wa mwanafunzi. Hata hivyo, walimu hawakuonekana kufuata mwelekeo huu; walijikita tu katika maelezo ya uvumbuzi ziarani bila kumpa mwanafunzi nafasi ya kueleza aliyoyaona na ugunduzi wake.

Mwangi (2013) anasisitiza ufundishaji ambao utawajengea wanafunzi umilisi ambao utawawezesha katika kukabiliana na changamoto za karne ya ishirini na moja, ambazo zinatokana na masuala mtambuko mabalimbali ambayo yanaweza kushughulikiwa na mwalimu kupitia ufundishaji bora; kupitia matumizi ya mbinu mwafaka za ufundishaji. Takwimu zilibainisha kuwa, 100% ya walimu walitumia mbinu ya mhadhara na ile ya maswali na majibu. Hali hii ina maana kwamba walimu walikosa ubunifu unaohitajika kuwawezesha kuteua mbinu anuwai na mwafaka za kufundishia masuala mtambuko. Ni vyema walimu wafahamu kuwa, uteuzi wa mbinu mwafaka unategemea ubunifu wao ili kuwezesha mwingiliano wa mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zitachangiana katika kukuza umilisi unaotarajiwa na hatimaye kufikia malengo ya ufundishaji.

## HITIMISHO

Makala haya yamechunguza na kutoa tathmini kuhusu ufundishaji wa masuala mtambuko katika shule za msingi. Imebainika kwamba matumizi ya mbinu mbalimbali za kufundishia kwa kiasi kikubwa yanatinga ufikiaji wa madhumuni ya ufundishaji wa masuala mtambuko katika shule za msingi za Kaunti ndogo ya Kimilili. Madhumuni ya ufundishaji yanastahili kuimarisha ufikiaji wa malengo ya elimu. Matokeo yameonesha kwamba ufundishaji wa masuala mtambuko unafanywa kwa kutumia mbinu za kimapokeo ambazo haziwashirikishi wanafunzi inavyopaswa. Aidha, imedhihirika kwamba walimu wanakosa kufanya maandalizi kabambe kabla ya zoezi la ufundishaji. Hili linachangia kuwepo kwa ukosefu wa kuzingatia vifaa na nyenzo faafu katika ufundishaji. Kutokana na matokeo haya, ili kuimarisha hali zilizopo, ufundishaji wa masuala mtambuko unastahili kutiliwa mkazo kupitia kwa matumizi fanikivu ya mbinu faafu za ufundishaji. Elimu ya walimu kuhusu ufundishaji ufaao wa masuala mtambuko yapaswa kuzingatiwa. Pia, matumizi ya vifaa mwafaka vya kufundishia masuala mtambuko vikiwemo vifaa halisi na vya kielektroniki vizingatiwe kikamilifu. Hatimaye, kuna haja ya kuwepo kwa tathmini ya mara kwa mara kuhusiana na viwango vya ufundishaji wa masuala mtambuko katika shule za msingi.

## MAREJELEO

Chang'ach, J. K. & Kessio, D. K. . (2012). Education for development: Myth or reality? The Kenyan experience. *International Journal of Learning and Development*, *2*(3), 114-163.

Chang'ach, J. K. & Kessio, D. K. (2012). Education for development: Myth or reality? The Kenyan experience . *International Journal of Learning and Development*, *2*(3), 114-163.

Gross, N. Giacquinta, J. B. & Berstein, M. (1971). *Implementing Organizational Innovation: A Sociological Analysis of Planned Educational Change.* New York: Basic Books.

Kassem, A. K. (1992). *Teacher perceptions of Agricultural teaching practices and methods for youths and adult in Lowa.* Lowa: Lowa State University.

KICD. (2017). *Lower Primary level curriculum design: Volume 1 Kiswahili, Literacy and Indegenous Languages, English Activities.* Nairobi: Author.

KICD. (2019). *Lower primary level curriculum design: Volume 1 Kiswahili, Literacy and Indegenous Languages, English Activities.* NairobI: Author.

Kumar, R. (2005). *Reserch Methodology: A step by Step Guide for Beginners* . London: Sage Publcations Limited.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

Magare, Y. D. (2011). *Matumizi ya majadiliano ya vikundi katika kufunza stadi ya kuzungumza katika shule za upili katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.* Nairobi: Kenyattta University.

Mbae, D. K. (2015). *Factors influencing implementation of Kiswahili curriculum in public primary schools in Igoji division, Meru county, Kenya.* Masters Thesis, University of Nairobi.

Mwangi, S. M. (2013). *Responsiveness of primary teachers education to challenges of the 21 century.* Phd thesis, Kenyatta University.

NCPPHE. (2008). *Partnerships for public purposes: Engaging higher education in societal challenges of the 21st century.* San Jose: National Centre fof Public Policy and Higher Education.

Ndege, J., Kea,P., Osoro, E., Waititu, F., Mucheria, Z. na Wafula, W. (2020). *Kiswahili Dadisi: Mwongozo wa Mwalimu Gredi ya 4.* Nairobi: Oxford University Press.

Nyokabi, K. J. (2018). *Teacher Factors Affecting the Implementation of Early Chilhood Development and Curriculum in Mathira East Sub- County, Nyeri County,Kenya.* Kenyatta University. Nairobi: unpubished .

Ondimu, S. M. (2018). *Teachers' preparedness for the implementation of the Competece Based Curriculum in private pre-schools in Dagoretti sub-county Nairobi city county .* Masters' thesis, University of Nairobi, Nairobi. Imechukuliwa toka http://www.res

Owala, O. R. (2021). Success and challenges of implementation of the Competence-Based Curriculum in Kenya.

Ransaw, T. S., & Majors, R. (Eds.). (2017). *Emerging issues and trends in education (International Race and Education Series).* Michigan: Michigan State University Press. doi:10.14321/j.ctt1qd8zjk

Schleicher, A. (2018). Educating learners for their future not our past. ECNU Review of Education. *1*(1), 58-75. doi:10.30926/ecnuroe2018010104

Sifuna,D, N. & Obonyo, M. M. (2019). Competence Based Curriculum in primary schools in Kenya: Prospect and challenges of implementation . *3* (7), 37-50.

UNESCO. (2000). *Education in the situations of emergency and crisis: Challenges for the new century.* Paris: Author.

UNICEF. (1999). *Education; The state of the Word's children.* Thailand: Author.

Wasike, M. W. (2015). *Tathmini ya matumizi ya nyimbo za kizazi kipya kama mbinu ya kufundishia masuala ibuka katika Kiswahili kwenye shule za upili nchini Kenya.* Kibabii University. Bungoma: Kibabii University.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.